ROHILA SECONDARY SCHOOL

CONTACTS:
0769 212 296
0755 306 466
0755 747 594

P.O. Box 1103,
MBEYA

Website: www.rohilaschools.sc.tz
Email Address: rohila_secondaryschool@yahoo.com

FOMU NA: _____
(Gharama ya fomu hii ni Tshs 10,000.00)

FOMU YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA ROHILA MWAKA 2019

SEHEMU A: MASOMO YANAYOFUNDISHWA

Civics, History, Geography, Kiswahili, English Language, Literature in English, Basic Mathematics, Additional Mathematics, Chemistry, Physics and Biology.

SEHEMU B: MCHANGANUO WA GHARAMA KWA MWAKA 2019
I: SARE YA SHULE KWA WAVULANA NA WASICHANA NA FEDHA YA MATUMIZI

- Sare ya shule kwa wavulana: Suruali 2, Sweta 2 kwa ajili ya sare ya darasani na Suruali 2, T-shirt 2, kwa ajili ya shamba dressing.
- Sare ya shule kwa wasichana: Sketi 2, Sweta 2 kwa ajili ya sare ya darasani na Sketi 2, T-shirt 2, kwa ajili ya shamba dressing. Sare zote zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tshs 150,000/= pamoja na kitambulisho cha shule.
- Fedha kwa ajili ya ziara mbalimbali za kimasomo (Study Tours) Shs 30,000/=
- Kabidhi fedha ya matumizi ya mwanao (Pocket money) Tsh. 25,000/= kwa mhasibu wa shule kwa muhula, ambapo mwanao atapatiwa sh 2,000/= kila wiki.
- Rimu moja A4.
- Jembe 1, fagio 1 na kwanja 1.

II: KARO YA SHULE NI TSHS 1,500,000/= KWA WANAFUNZI WA HOSTEL NA TSHS 600,000/= KWA WANAFUNZI WA KUTWA

Karo ilipwe kwa awamu **NNE AUMBILI** kama ifuatavyo kwa wanafunzi wa hostel na kutwa:

S/N	Hostel	Kutwa	Muda wa kulipa
i.	500,000.00	300,000.00	Lipa kabla ya shule kufungua January, 2019
ii.	250,000.00		Lipa mwezi March 15, 2019
iii.	500,000.00	300,000.00	Lipa kabla ya Julai Mosi, 2019
iv.	250,000.00		Lipa mwezi Septemba 15, 2019

NB: Shule itafungua tarehe 6 Januari 2019 Siku ya Jumapili.

TAFADHALI ZINGATIA YAFUATAYO*:*

- Kulipa ada na michango mingine kwa wakati uliopangwa
- Lipa kupitia akaunti ya shule **0150422076700 iliyopo CRDB Bank.** Fedha tasilimu haitapokelewa shuleni.
- Hakikisha 'Original Bank pay slip' (risiti ya Benki original) anakuja nayo mwanafunzi pindi anaporipoti.
- Ikiwa Mwanao anayo kadi ya Bima ya Afya, aje nayo ili aitumie pindi anahitaji matibabu.

- **FEDHA YA MATUMIZI YA MWANAFUNZI**

  Wazazi wanaweza kutuma fedha ya matumizi ya Mwanafunzi kwa M-Pesa kupitia namba 56 53 785 kwa kufuata hatua zifuatazo:

  1. Piga *150*00#
  2. Chagua Namba 4. (LIPA kwa M-Pesa)
  3. Chagua Namba 1 (Weka LIPA Namba
  4. Weka Namba 3653785
  5. Weka Kiasi cha kutuma
  6. Bonyeza Namba 1 (Kuthibitisha)

  Baada ya kukamilisha muhamala tuma ujumbe mfupi kwenda namba **0764705320** unaojulisha Jina la Mtumaji, Kiasi na Mlengwa (Jina la Mwanafunzi).

- Ada au fedha ya matumizi isitumwe kwa mwalimu au mfanyakazi yeyote wa shule.

III: MAHITAJI MENGINE YA MWANAFUNZI ANAYOTAKIWA KUJA NAYO NI KAMA YAFUATAYO*:*

i) Shati nyeupe 2 zenye mikono mirefu na Tai 2 (Light blue).

ii) Picha ndogo 4 (passport size).

iii) Nguo za michezo (tracksuit ya blue au nyeusi, raba na T-shirt bluu).

iv) Viatu vyeusi vyenye kisigino kifupi na vya kamba jozi mbili.

v) Mwanafunzi aripoti akiwa amevaa suruali kwa wavulana na sketi ndefu zisizobana kwa wasichan na suruali/sketi nyingine mbili ndefu zisizobana za ziada kwa ajili ya kuvaa akisubiri kushonewa sare ya shule.

vi) Vyombo vya huduma ya chakula k.m. Sahani, Bakuli, kijiko, kikombe cha uji na kupigia mswaki.

vii) Vifaa vya kuogea k.m. Ndoo ndogo, Taulo, Sabuni za kufulia, Sabuni za kuogea n.k

viii) Godoro la ft 6 kwa nch "2 ½ "

ix) Blanketi 1, shuka mbili za rangi ya Pink 1pc, light Blue 1pc na chandarua 1pc

x) Soksi nyeupe zenye urefu wa kati, jozi 3 na Toilet paper 6pc.

xi) Vifaa vya darasani k.m. kamusi ndogo ya kiingereza, madaftari aina ya KAUNTA (11pcs), Mkebe, Rula, kalamu ya risasi na file box 1.

SEHEMU C: ANGALIZO KWA MZAZI/MLEZI

i) Fedha yeyote itakayo lipwa kwa Mhasibu haitarudishwa tena kwa mteja.

ii) Mawasiliano yoyote kati ya Mwanafunzi na mtu nje ya shule tafadhali yafanyike kwa kupitia uongozi wa shule. **Mwanafunzi haruhusiwa kuwa na simu ya mkononi.**

iii) Mwanafunzi aripoti shuleni na mavazi yenye heshima, asije na suruali/sketi, T-shirts zenye maandishi, nguo inayobana, fupi au ya kuangaza.

iv) Mwanafunzi asipewe vitu vinavyo weza kumsababishia akafanya mambo ya anasa. Sambamba na hilo Mzazi /Mlezi unashauriwa kutompatia mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apoteze utulivu wa maisha ya shule na kuvunja sheria. Pesa zote za wanafunzi zitatunzwa kwa mhasibu wa shule, na atatia sahihi anapozichukua.

v) Shule ina utaratibu wa kuandaa usafiri wa kuwarudisha wanafunzi wakati wa kurudi makwao kwa safari (route) ndefu, hivyo Mzazi utatakiwa kukabidhi nauli na posho ya njiani shule ifungapo.

vi) Mtoto akishapokelewa shuleni, Mzazi huruhusiwi kuja kumuona mtoto labda uitwe na uongozi wa shule au kwa ombi maalum toka kwa Mzazi lenye manufaa kwa mwanafuzi. Kwa hiyo, hapatakuwa na **VISITING DAY**.

vii) Ni wajibu Mzazi kuhakikisha mwanafunzi amefikishwa shuleni kwa wakati anaotakiwa.

EDUCATION FOR INNOVATION

SHERIA ZA SHULE

1. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu walimu/wafanyakazi wote na mtu yeyote aliyemzidi umri awapo shuleni na mahali pengine popote pale. Pia mwanafunzi hatakiwi kutoa zawadi kwa mtumishi ye yote awapo shuleni au atokapo likizo. Mwanafunzi atakayeenda kinyume na sheria hii **ATAADHIBIWA**.

2. Ni lazima mwanafunzi aoneshe nidhamu ya kiwango cha juu katika maongezi na mwanfunzi mwenzake, wazazi wake/ walezi wake bila kutumia lugha ya matusi/chafu/ mtaani/ kejeli/ ubishi/ dharau/kuzomea/kufyonza. Kushindwa kufanya hivi kutasababisha mwanafunzi kupewa onyo kali au **KUSIMAMISHWA MASOMO/KUFUKUZWA SHULE** au vyote kwa pamoja.

3. Mwanafunzi anatakiwa kuishi kwa amani, heshima, utii, usikivu, na upendo kwa watu hivyo hapaswi kupiga/kupigana kushiriki uovu wa aina yoyote ile popote ikiwa ni kwa kuona/kusikia. Ni wajibu wake kutoficha siri ya ouvu wowote aliouona/kuusikia, kupatikana na kosa lolote katika haya kutasababisha mwanafunzi huyu kuadhibiwa kwa **KUSIMAMISHWA MASOMO**/ **KUFUKUZWA SHULE BILA MSAMAHA.**

4. Mwanafunzi akikamatwa na makosa yafuatayo: wizi, ulevi, uvutaji sigara, uasherati, kufanya mapenzi nje na ndani ya shule, kujihusisha na mazungumzo ya mapenzi, kusagana, kupata mimba/kutoa mimba, kutoroka au kulala nje ya shule, kuingia kwenye vilabu vya pombe/ kumbi za starehe, kutumia madawa ya kulevya, na kuandikiwa barua ya mapenzi. Kwa kosa lolote katika hayo, mwanafunzi **ATAFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA BILA MSAMAHA.**

5. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia, viatu vyenye kisigino kirefu, visivyo na kamba, heleni mikufu, kanga, bangili, pete, sketi fupi za kubana/ mipasuo. Marufuku kufuga nywele, kupaka rangi kucha au nywele, kujichubua, Yeyote atakayepatikana na haya atarudishwa nyumbani **KUMLETA MZAZI AU MLEZI PAMOJA NA ONYO KALI**.

6. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu, redio, kamera, CD, DVD, pasi, hita, Mshumaa, kiberiti na silaha yoyote mfano Kisu, chupa. Aidha kuwa na dawa za aina yeyote bwenini, kwa kila kosa adhabu yake ni **KUFUKUZWA SHULE BILA MSAMAHA.**

7. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare wakati wote awapo darasani, atokapo nje ya shule aendapo kanisani / msikitini aingiapo shuleni, anaposafiri kuja shuleni na aendapo hospitalini. Kushindwa kufanya hivyo ni kosa linalosababisha mwanafunzi **KUFUKUZWA/KUSIMAMISHWA SHULE.**

8. Shule inafuata maadili ya Kikristo na inapokea wanafunzi wa Dini zote, mwanafunzi wa dhehebu/dini yoyote anatakiwa kufuata taratibu na sheria za shule kuhusiana na ibada na malezi. Ni maarufuku kwa mwanafunzi kubadilisha imani ya Dini ya Wazazi wake bila ya idhini ya Wazazi wake. Kufanya kinyume na hili **ADHABU KALI ITACHUKULIWA DHIDI YAKE**.

9. Ni marufuku mwanafunzi kuletewa chakula chochote kutoka nje ya shule kwa sababu za kiusalama. Pia haruhusiwi kupokea na kuongea na mgeni yeyote, isipokuwa Mzazi au Mlezi aliyeandikishwa na kutambuliwa na ofisi ndiye anayeweza kuonana na mwanafunzi ikiwa ulazima utajitokeza. Aidha, Mzazi/ Mlezi haruhusiwi kuonana na mwanafunzina. Akikiuka sheria hii **ADHABU KALI ITACHUKULIWA.**

10. Ni lazima mwanafunzi aripoti shule inapofunguliwa na isizidi saa kumi jioni. Pia mwanafunzi anayechelewa kwa siku na muda uliopangwa hatapokelewa badala yake **ATARUDISHWA NYUMBANI KUMLETA MZAZI.**

11. Ni wajibu wa mwanafunzi kushiriki kazi za mikono kama Usafi wa mazingira, kufyeka (kufagia), ujenzi, kilimo, n.k. Kukataa kufanya hivyo **ADHABU KALI ITATOLEWA/KUMLETA MZAZI.**

12. Mwanafunzi haruhusiwa kuvaa ndala popote isipokuwa awapo bwenini tu. Kukiuka sheria hii, **ADHABU ITATOLEWA.**

13. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa, Fedha na picha za Viongozi na alama nyingine za Taifa na kuheshimu miito yote ya kengele. Kutofanya hivyo **ADHABU KALI ITACHUKUKIWA**.

14. Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi wakati wote, kulala katika sehemu aliyopangiwa kwa wakati unaotakiwa, kutolala wawili katika kitanda kimoja na kuhakikisha kuwa bweni na darasa lake ni safi wakati wote ikiwa ni pamoja na sehemu ya kulia chakula na ukumbi. Kushindwa kufanya hivyo ni kosa na **ADHABU ITATOLEWA.**

15. Mwanafunzi haruhusiwa kufanya mawasiliano na Mzazi/Mlezi bila ruhusa ya uongozi wa shule. Pia mwanafunzi anatakiwa kuomba kibali maalum endapo kutakuwa na tatizo litakalomlazimu mwanafunzi kuhudumiwa nje ya shule. Kutofanya hivyo kutasababisha **KUSIMAMISHWA SHULE/KUMLETA MZAZI.**

16. Mwanafunzi anatakiwa kufanya bidii sana katika masomo awapo shuleni. Mwanafunzi mvivu hatavumiliwa, endapo atashindwa kufikisha kiwango cha alama zilizowekwa na uongozi wa shule (wastani wa alama **50** kidato cha kwanza kwenda cha pili na cha pili kwenda cha tatu. Na wastani wa kidato cha tatu kwenda cha nne lazima mwanafunzi afikishe alama ya daraja la ***pili*** katika ufaulu, vinginevyo **ANAPASWA KUMLETA MZAZI**).

17. Mwanafunzi anatakiwa kuwa kimya wakati wote anapokuwa katika mazingira ya shule (yani darasani, Bwenini, Mesini) na asitoke bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo. Aidha, mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shule muda wote wa masomo ndani na nje ya darasa (ruhusa yoyote ya kutohudhuria darasani itatolewa na Mkuu wa shule tu au mwalimu akatakayekuwa ameteuliwa na Mkuu wa shule mfano: Makamu Mkuu wa shule, Mwandamizi Taaluma, Nidhamu n.k. Kukaidi hayo ni makosa, hivyo mwanafunzi anaweza **KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE**.

18. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria na kuheshimu maandalizi ya jioni na asubuhi (Night na Morning preparations) kushindwa kufanya hivyo mwanafunzi anatakiwa akamlete Mzazi/Mlezi na **ADHABU KALI ITATOLEWA**.

19. Mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya atatakiwa aoneshe cheti cha tatizo lake kutoka kwa Daktari wa hospitali ya serikali. Kinyume na hivyo **AMLETE MZAZI/MLEZI**.

20. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika maandishi kitabuni, katika dawati, meza, viti au kwenye kuta za majengo ya shule. Kukaidi kutii hili ni makosa, hivyo mwanafunzi anaweza **KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE.**

21. Mwanafunzi akifukuzwa shule au kuacha shule ada yake haitarudishwa.

22. Mawasiliano yote ya mwanafunzi awapo shuleni yatakuwa kwa lugha ya **KIINGEREZA** hivyo ni wajibu wake kujifunza lugha hiyo kwa bidii na kuongea muda wote. Kutozingatia hilo, mwanafunzi atarudishwa nyumbani kumleta Mzazi na **KUPEWA ONYO KALI.**

23. Matatizo au mapendekezo yawasilishwe kwa kupitia serikali ya wanafunzi, sanduku la maoni au uongozi wa shule pawapo na tatizo lolote kwa ufumbuzi wa mara moja. Uongozi hauta mvumilia mwanfunzi yeyote akakayejihusisha na

maandamano au migomo ya aina yoyote ile. Kufanya kosa hilo kutasababisha mwanafunzi **KUFUKUZWA SHULE MOJA KWA MOJA BILA MSAMAHA.**

24. Ni lazima mwanafunzi aamke na kulala kwa wakati na muda uliopangwa na uongozi wa shule, vinginevyo mwanafunzi atarudishwa kumleta Mzazi/Mlezi wake na **ADHABU ITATOLEWA DHIDI YAKE.**

25. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kulinda mali zote za shule kama dawati na meza anayokalia, vifaa vya usafi, kutokuharibu majengo ya shule (kuta, milango na madirisha) kuacha mabomba wazi, kuacha taa zinawaka na samani zote, vinginevyo **ITAMLAZIMU KULIPIA**. Kushindwa kufanya hivyo atapaswa **KUMLETA MZAZI.**

26. Mwanafunzi haruhusiwi kukata mti katika mazingira ya shule, pia ni wajibu wake kutunza mazingira hayo kwa kuokota karatasi pale anapoona na kutotupa karatasi ovyo, kushindwa kufanya hivyo kutafanya mwafunzi **KUSIMAMISHWA MASOMO AU KULIPIA MTI ALIOKATA AU VYOTE KWA PAMOJA**.

27. Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria darasani muda wote wa masomo awapo shuleni hivyo hatakiwi kuonekana bwenini wakati wa vipindi/ masomo pasipo ruhusa kutoka kwa uongozi wa shule, vinginevyo **ATARUDISHWA NYUMBANI KUMLETA MZAZI NA ADHABU ITATOLEWA.**

28. Mwanafunzi haruhusiwi kudanganya katika mitihani yoyote ile iwe ya ndani au nje. Kufanya kosa hilo kutasababisha mwanafunzi **KUFUKUZWA SHULE BILA MSAMAHA.**

29. Ni marufuku mwanafunzi kutembelea au kuingia vyumbani kwa walimu au wafanyakazi wasio waalimu bila ruhusa maalumu, pia haruhusiwi kuingia jikoni isipokuwa kwa kibali maalum. Kukaidi hili **HATUA KALI ZA KINIDHAMU ZITACHUKULIWA PAMOJA NA KUMUITA MZAZI.**

30. Ni kosa kwa mwanafunzi kumkimbia mwalimu au mfanyakazi yeyote aidha kumgomea mwalimu, kiongozi asiye mwalimu. Kosa hili litamsababishia mwanafunzi **KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE**.

31. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia muda uliopangwa, hii ni pamoja na kuwepo eneo husika kwa muda husika vinginevyo **ADHABU KALI ITATOLEWA JUU YAKE**.

32. Mwanafunzi haruhusiwi kuingia na chakula bwenini /darasani na sehemu yoyote isiyo rasmi kulia chakula. **KUFANYA HIVYO ADHABU KALI ITATOLEWA**.

Mimi …… nimesoma na kuzielewa sheria za shule. Nakubali kwamba nitazingatia na kuzitii mara nipatapo nafasi ya kujiunga.

Weka sahihi hapa……tarehe……..

MEDICAL EXAMINATION

(Fomu hii ijazwe na Daktari wa Hospitali za Serikali tu)

A. Hospital Name: .....

B. District: ..... Regional: .....

S/N	DISEASES/CAUSES	OBSERVATION RESULTS	REMARKS
1	Skin Diseases		
2	Pregnancy case		
3	Urine		
4	Blood		
5	Chest		
6	Eyes		
7	Ears		
	Any chronic disease?	i. ..... ii. ..... iii. ..... iv.	

C. Other Cases

i. Does she/he select food due to stomach pain? (YES/NO).....

ii. Does she/he experience headache pain? (YES/NO).....

D. General comments

That the examined student..... (name) is (fit/unfit)

or

i. .....

I certify that the information provided above is true and correct.

Doctor's name.....

Signature: .....

(Hospital stamp)

EDUCATION FOR INNOVATION